JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
Ofisi ya Rais
Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
Shule ya Sekondari Mwabusalu

Phone: +255 629515553/ +255 768102798
P. O. Box 232
Meatu - Simiyu

KUMB. NA. MSS/BR 1/KDT I/2020/01

15/12/2020

Mzazi/ Mlezi wa ……………………………………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MWABUSALU MWAKA 2021**

**UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari **Mwabusalu.** Shule iko umbali wa kilometa 71 Kaskazini Magharibi mwa wilaya ya Meatu. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 saa 1:00 Asubuhi na mwisho wa kuripoti ni tarehe 15/01/2021. Hivyo ni vyema kuzingatia muda huo.

**1. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**1.1. SARE ZA SHULE**

**A. WAVULANA**

- Suruali mbili rangi ya kijivu iliyo na malinda mawili na isiyobana na mashati mawili meupe yenye mikono mifupi
- Viatu vya ngozi rangi nyeusi vyenye kamba, visivyochongoka na visivyo na soli kubwa
- Soksi (stocking) rangi nyeusi ndefu
- Tai rangi ya kijivu
- Mkanda wa suruali mwembamba rangi nyeusi
- Pull-over (sweta) rangi ya blue kwa ajili ya baridi **SIYO** lazima

**B. WASICHANA**

- Sketi mbili za rangi ya kijivu yenye **urefu kasoro sentimita kumi na tano (sm 15) kugusa ardhi** na iwe na linda box moja kwa mbele na nyuma na mashati meupe mawili ya mikono mifupi.
- Viatu vya ngozi rangi nyeusi vyenye kamba, visivyochongoka na visivyo na soli kubwa
- Soksi (stocking) rangi nyeupe ndefu
- Skafu ya rangi ya kijivu.
- Hijab rangi nyeupe kwa wasichana wa kiislamu ruksa.
- Pull-over (sweta) rangi ya blue kwa ajili ya baridi

**SARE ZA MICHEZO**

Shule hii inasisitiza michezo kwa afya na makuzi bora. Hivyo uje na vifaa vifuatavyo

i. Bukta moja rangi blue, T-shirt isiyokuwa na kora, rangi ya zambarau kwa wasichana na wavulana
ii. Viatu vya raba vya michezo (rangi yoyote)



Scanned with CamScanner

## 1.2MAHITAJI MENGINE MUHIMU YA KUJA NAYO

- Daftari kubwa 12 (kumi na mbili)
- Kalamu za wino 2 (blue/black)
- Kalamu za risasi za kutosha
- Mkebe wa vifaa vya hisabati (Mathematical set)
- Begi la kuhifadhia daftari **(mfuko wa Rambo hauruhusiwi)**
- Ndoo ndogo moja (1) ya lita 10 **kwa wavulana na wasichana kwa ajili ya usafi**

**NI MUHIMU:** Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa msafi kimwili, kimavazi, kiroho, kuwa na nywele safi na fupi. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi wa shule kusuka, kunyoa panki, kipara, kutinda, kuchonga au vitu vingine vya mapambo havipaswi kuvaliwa na mwanafunzi anapokuwa ndani na nje ya shule.

## 2. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

2.1. Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha shule hii inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu, unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa Nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio na mazoezi mbalimbali ya kitaaluma yatakayotolewa na mwalimu darasani.
d) Kuwahi katika shughuli utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwapo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote vipindi vinapoendelea.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
h) Kutunza mali za umma

2.2. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa shule au kusimsmishwa shule.

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi, matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocain, mirungi, kuberi n.k
e) Kupigana na kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali umma
g) Kudharau bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba/kumpa mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
k) Kukataa adhabu kwa makusudi
l) Kumiliki simu ya mkononi, laini, charger, pamoja na vitu vingine vya kufanana na hayo
m) Kukosa kuhudhuria vipindi darasani au kutofanya mitihani na majaribio kwa makusudi

**NB:** Viatu vya madaso/raba havitakiwi, maelekezo yafuatwe kam
a yalivyo.

2.3. Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA NA KARIBU SANA MWABUSALU SEKONDARI**

..............................................

**JUDITH K. MATATIZO**

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
MWABUSALU SEKONDARI
MEATU



Scanned with CamScanner

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**Ofisi ya Rais**

**Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

**Shule ya Sekondari Mwabusalu**

P. O. Box 232

**Phone: +255 629515553/ +255 768102798** Meatu - Simiyu

## SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Sheria na kanuni hizi zinazingatia misingi ya **HESHIMA, ADABU, UAMINIFU, UTII** na **TABIA NJEMA** kwa ujumla.

Wanafunzi wanatazamiwa kuwa mfano mzuri kwa heshima na tabia, kauli na vitendo, hivyo:

1. Mwanafunzi atasimama anapomsalimu mwalimu, mtumishi wa shule au mtu yeyote aliyemzidi umri
2. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kutumia lugha chafu na ya kihuni, mahali popote na wakati wowote hata kwa wanafunzi wenzake.
3. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi
   (a) Kufuga kucha na nywele
   (b) Kufuga ndevu
   (c) Kunyoa kipara
   (d) Kutukana
   (e) Kutia dawa nywele (curly) na kujichubua ngozi ya mwili kwa madawa
   (f) Kuvaa vitu kama mapambo mfano heleni, mikufu, bangili au vitu vya kiimani kama vile Rozali.
   (g) Kuvaa kofia, kanzu, vilemba, suruali fupi kwa kuwa shule hii ni ya serikali
   (h) Kuvaa viatu vya soli nene na ndefu
   **(i)** Kuvaa **suruali chini ya kiuno**
   (j) Kuvaa kaptula na kanda mbili katika eneo la shule
   (k) Kuvaa nguo za mtindo, mfano **model au jins**
4. Mwanafunzi atanyoosha mkono juu na kusimama anapouliza au kujibu swali akiwa darasani au mikusanyiko ya kishule kama ilivyoamuliwa
5. Anatakiwa kuwa mtulivu asipige kelele au vitendo vyovyote vitakavyosababisha usumbufu kwa wengine anapokuwa darasani,bwenini, maktaba,wakati wa kujisomea (prepo) na katika mikusanyiko yoyote mfano paredi n.k
6. Mwanafunzi **LAZIMA** awahi na ahudhurie mahali anapotakiwa katika shughuli za shule. Hivyo mwanafunzi:-
   (a) Aripoti shuleni tarehe ya kufungua shule na kijiandikisha rasmi siku na saa ya kuripoti kwa mwalimu anayehusika
   (b) Ahudhurie vipindi vyote darasani kama ilivyoopangwa
   (c) Ahudhurie kwenye kazi atakazopangiwa
   (d) Ahudhurie paredi kila siku
7. **NI LAZIMA** mwanafunzi awe katika sare ya shule kwa nyakati zote awapo shuleni na nje ya shule kama:
   Anapotoka nje ya shule kwa ruhusa maalumu itakayomlazimu kwenda nje ya shule
8. NI LAZIMA mwanafunzi awe ndani ya mipaka ya shule wakati wote isipokuwa akiruhusiwa kuwa nje ya mipaka ya shule kwa ruhusa maalumu, atapaswa kuwa na kibali cha maandishi
9. Hairuhusiwi kufanya mikutano yoyote shuleni pasipo kibali cha mkuu wa shule na ikiwa kibali kimetolewa, kikundi au chama kitatakiwa kuandika muhtasari wa kikao na nakala kurudishwa kwa mkuu wa shule
10. USAFI: Mwanafunzi atawajibika kuwa msafi kwa mavazi na mwili wake na kushiriki kuyaweka mazingira ya shule katika hali ya usafi
11. Hiruhusiwi kijihusisha na mikutano ya siasa katika kipindi chote awapo mwanafunzi

Scanned with CamScanner

## 12. MAENEO YASIYORUHUSIWA:

Mwanafunzi haruhusiwi kufika /kuingia sehemu zifuatazo bila ruhusa maalumu

a. Ofisi za shule
b. Bohari za shule (stoo ya chakula)
c. Kwenye disco,ngoma,mziki
d. Maabara
e. Baa, kilabuni au mahali popote panapouzwa pombe au vileo vingine
f. Nyumba za wageni (Guest House)
g. Nyumba za watumishi/walimu

## MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE

1. Wizi
2. Uashereti, ushoga na ulawiti
3. Ulevi wa aina yeyote
4. Utumiaji wa madawa ya kulevya
5. Uvutaji wa sigara au bangi
6. Makosa ya jinai
7. Kuoa au kuolewakuharibu kwa makusudi mali ya umma
8. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
9. Kupigana au kumpiga mwingine
10. Kudharau bendera ya Taifa
11. Kuchochea au kufanya vurugu au kugoma kwa namna yoyote
12. Kutoa lugha ya matusi
13. Kumdharau kiongozi wa shule, mwalimu, mfanyakazi na jamii kwa ujumla
14. Kutohudhuria vipindi
15. Mwanafunzi kumiliki simu au sehemu ya simu kama laini, charger n.k



Scanned with CamScanner

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

## President's Office

## Regional Administration and Local Government

## Mwabusalu Secondary school

P. O. Box 232

**Phone: +255629515553/ +255 768102798** **Meatu- Simiyu**


### STUDENT'S MEDICAL REPORT FORM

**PART I: Student's report personal details**

Student's name ..............................................................................

Age ............................... Age ..................................

**PART II: Medical report**

Are you suffering or have suffered from any of the following? Indicate **YES** or **NO**

1. Tuberculosis ...............................................................................................
2. Asthma ...............................................................................................
3. Rheumatic fever ...............................................................................................
4. Allergic disorders ...............................................................................................
5. Heart disease ...............................................................................................
6. Dysentery ...............................................................................................
7. Viscose veins ...............................................................................................
8. Kidney disease ...............................................................................................
9. Diabetes ...............................................................................................
10. Epilepsy ...............................................................................................
11. Deformity ...............................................................................................
12. Mental illness ...............................................................................................
13. Eye Disorder ...............................................................................................
14. Ear, Nose or Throat disorder ...............................................................................................
15. Skin disease ...............................................................................................
16. Anemia ...............................................................................................
17. Gynecological disorder ...............................................................................................

    Additional information: example physical defects or impairments infections, chronics or family disease etc

    ...............................................................................................................................

    ...............................................................................................................................

**PART III: Conclusion**

I have personally examined Mr. / Miss ................................................................................ and consider that He or She is physically and mentally fit/ unfit to be admitted to the school for studies.

**Name and signature of certifying Officer.**

Name ................................................................................ Signature ..................................................

Station ................................................................................ Destination ..................................................

Date ................................................................................ Stamp ..................................................



Scanned with CamScanner

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## Ofisi ya Rais

### Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

### Shule ya Sekondari Mwabusalu

P. O. Box 232
Phone: +255629515553/ +255 768102798 Meatu - Simiyu

**FOMU YA KUANDIKISHWA SHULE NA AHADI YA UTII**

KIJIJI CHA ..............................................
S.L.P .......................................
MWANHUZI-MEATU.
TAREHE .........................

(Ijazwe kwa herufi kubwa na irudishwe kwa mkuu wa shule)

1. (a) Jina kamili ..............................................................................................
   (b) Tarehe ya kuzaliwa ..............................................................................
   (c) Kijiji/kata ..........................................................................................
   (d) Shule uliyotoka ...................................................................................
2. Jina kamili la baba/mama/mlezi .......................................................
   Anuani yake/simu ....................................................................................
   Kazi ya baba/mama/mlezi ..........................................................................
3. Ahadi ya mwanafunzi:
   Mimi .................................................................................................. nimeyasoma na kuyaelewa maelekezo yote ambayo ni pamoja na sheria za shule. Nayakubali na niko tayari kuwa mwanafunzi wa shule ya sekondari **MWABUSALU**
   Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu na ni nyeti kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya Taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwa ajili yangu pia.

   **Naahidi kwamba:**

   i. Nitatimiza masharti yote ya shule
   ii. Nitatimiza sheria zote za shule. Nikikiuka ahadi zangu nichukuliwe hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule

   Saini ya mwanafunzi ......................................... Tarehe ....................................................
4. Ahadi ya mzazi/mlezi
   Mimi ................................................................................................ mzazi/mlezi wa mwanafunzi huyu naahidi kwamba;

   i. Nitashirikiana kikamilifu na uongozi mzima wa shule katika kumuelimisha na kumlea ipasavyo
   ii. Nitatimiza mahitaji yake ya shule
   iii. Sitamkatiza masomo kwa ajili ya shughuli za kifamilia, kumuoza/kumuozesha au mambo mengine kama hayo yawezayo kumfanya aache shule
   iv. Nitafanya kila jitihada kumwezesha mwanafunzi kuwahi shule kila siku na kufika shule siku ya kufungua shule bila kuchelewa
   v. Nitafuatilia maendeleo yake ya kitaaluma na tabia kila muhula bila kukosa.

Sahihi ya mzazi/mlezi .......................................
Tarehe ....................................

**Mawasiliano**

Namba za simu:.........................................au ................................

Scanned with CamScanner